

DMU

Halmshauri hii 03/07/2012  
wasi kutafuta taarifa  
hizi kwa taasisi  
isiyo ya serikali  
9/7/20

Sikika/149/2012

Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya Wilaya ya Iramba,  
Singida.

Ndugu,

**YAH! MAOMBI YA NAKALA ZA RIPOTI ZA UTEKELEZAJI WA MIPANGO YA VITUO  
VYA HUDUMA ZA AFYA KWA MWAKA 2010/11**

Tafadhali rejea kichwa cha Habari hapo juu.

Sikika ni asasi isiyo ya kiserikali inayolenga kuchochea uwazi na uwajibikaji katika sekta za afya na UKIMWI ili kuboresha huduma za afya nchini Tanzania.


Moja ya shughuli za Sikika ni kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mipango ya afya katika vituo vya huduma za afya vya umma, kwa lengo la kukuza ufanisi katika mipango na bajeti ili kuboresha upatikanaji wake kwa wananchi.

Kutokana na ongezeko la upungufu wa dawa na vifaa tiba katika vituo vya huduma za afya vya umma, Sikika inadhamiria kufanya mapitio ya ripoti za utekelezaji wa mipango ya afya unaofanywa na vituo vya huduma ili kubaini changamoto ambazo vituo vinakutana nazo katika maunizi ya fedha hususani za dawa na vifaa tiba. Lengo letu ni kutafuta ufumbuzi wa changamoto hizo ili kuboresha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba kwa umma.

Kwa barua hii Sikika inaomba ushirikiano na ofisi yako ili iweze kupata nakala za ripoti hizi zifuatazo:

- Mpango Mkakati wa Halmashauri 2010/2011
- Ripoti ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali 2010/2011
- Ripoti ya ndani ya Ukaguzi 2010/2011
- Vitabu vya bajeti 2010/2011
- Taarifa/Ripoti ya Utekelezaji 2010/2011

Tunatanguliza shukrani zetu kwako tukitegemea kupata ushirikiano wako.

  
Irenei Kiria  
Mkurugenzi Mtendaji

